

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz



S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

24 Julai, 2024

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YATOA USHIRIKIANO UENDESHAJI
MASHAURI YA SERIKALI MBEYA

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepongezwa na Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya kwa ushirikiano katika uendeshaji mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

Hayo yameelezwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Mhe. Joachim Tiganga wakati wa ziara ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo alipofika ofisini kwake wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Mbeya.

"Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Mbeya inatupa ushirikiano wa kutosha katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali Mbeya kwa kuwa Mkoa huu una mashauri mengi ukilinganisha na mikoa mingine ambapo baadhi ya mashauri yana maslahi mapana kwa taifa hivyo Mahakama kwa kushirikiana na Ofisi hii tunapenda kuendesha mashauri na kuyamaliza kwa wakati," amesema Mhe. Jaji Mfawidhi Tiganga.

Naye Bi. Mtulo amesema kuwa lengo la ziara hiyo ni kukagua utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoa wa Mbeya, kuonana na wadau na kufahamu masuala yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa mashauri.

Akiwasilisha taarifa ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mbeya, Wakili wa Serikali Mfawidhi, Allan Shija alisema kuwa *tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Mbeya mwaka 2018, jumla ya mashauri 361 yaliendeshwa, mashauri 259 yalimalizika na 102 yanaendelea ambapo asilimia 40 ni mashauri ya ardhi, 38% ya madai, 15% mashauri ya maombi yaliyoongezewa muda, 4% mashauri ya kazi, na 3% ya mashauri ya maombi ya gharama.*

Aliongeza kuwa kati ya mashauri hayo 102, mashauri 74 yapo Mahakama Kuu ya Tanzania, 24 Mahakama ya Rufani, mashauri 2 yapo Tume ya Usuluhishi na Upatanishi, mashauri moja (1) yapo Mahakama ya Wilaya Mbeya na lingine moja lipo Mahakama ya Wilaya Tunduma.

Prisca J. Ulomi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini